

# Pambazuko

Toleo Namba 070

Jumatatu Aprili 22-28, 2024

## Matumizi ya mbegu za vinasaba kiama

- *Nchi tajiri zahimiza majaribio kwa masikini, zazuia kwa watu wake*



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, Plasduce Mbossa*

**Tanga kuchele! Bandari yazaliwa upya-**

**UK. 14**

**Elimu ya mafao kinga dhidi ya 'majanga' ya ustaafu**

**UK. 19**

**Tunahitaji miaka mingapi kuimarisha Muungano?**

**UK. 17&18**



**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

## Tahariri

## Ni wakati Rais Samia kutimiza ahadi

**M**EI 3, ya kila mwaka, dunia huadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari.

Ni siku muhimu ambapo wadau wa sekta ya habari hukusanyika na kutathmini maendeleo, mwenendo na matarajio ya vyombo hivyo kwa ustawi wa jamii vinamofanya kazi.

Katika siku hiyo, pamoja na mambo mengine, uhusiano wa vyombo vya habari na serikali pia hupimwa ili kupata majibu endapo kuna mazingira wezeshi, rafiki na yenye uhuru unaotarajiwa.

Ni kutokana na mantiki hiyo, sisi Pambazuko tumeamua mwaka huu kupima utekelezaji wa ahadi za Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa na utayari wa wazi kufanya kazi na vyombo vya habari.

Rais Samia amekuwa akisisitiza kuwepo mazingira yenye kuwapa fursa waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa uhuru bila kughudhiwa na vyombo vya usalama ama taasisi za serikali anayoiongoza.

Kiongozi huyo wa Tanzania amekuwa akisema serikali anayoiongoza itahakikisha inaweka mazingira mazuri kwa waandishi wa habari kufanya kazi zao, huku akieleza kufuatwa kwa maadili ya tasnia hiyo kwa kuandika ukweli na kutoonea mtu.

Hata hivyo, pamoja na ahadi hizo nzuri, bado kuna ukakasi ambao unaweza kukwamisha nia – tunayoamini ni nzuri, ya Rais Samia na serikali yake; kwa kutokuwepo katika sheria, kanuni na sera.

Bila matamania ya Rais Samia kuwemo kwenye sheria, sera,

kanuni na miongozo mingine, upo uwezekano wa tasnia ya habari, hata kama inafanya kazi kwa weledi na kufuata sheria za nchi, ikashindwa kutoa mchango wake mkubwa kwa nchi kwa kuogopa kutishwa, kufungwiwa, kupelekwa mahakamani kwa sababu za hovyoy.

Ikumbukwe kuwa vyombo vya habari vya Tanzania vilipitia nyakati ngumu zaidi kupata kutokea kwenye historia ya nchi hii; kipindi cha utawala wa Rais John Magufuli ambaye aliamua kuwa mbabe kwa vyombo vya habari.

Pamoja na nia tunayoiona kuwa njema ya kuwapa haki na uhuru waandishi wa habari, ni vyema serikali ikaharakisha mchakato wa kuwepo sera na sheria ambazo zitabeba hayo anayoahidi Rais Samia.

Ieleweke kuwa kuwepo kwa sera na sheria zisizokandamiza utendaji wa waandishi wa habari, ni dhahiri maendeleo ya Tanzania yataongeza kasi kwani mchango wa sekta ya habari ni mkubwa mno, hata kama haupigiwi ‘chapuo’ na wanasiasa wengi.

Pambazuko linaamini kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ni mpenda haki, hivyo anakwenda kusimamia jambo hili lifanyike mapema naye apate mwanya wa kutambua yanayoendelea nje ya wigo rasmi wa kupokea taarifa na habari za utendaji wa serikali na hata maeneo mengine.

Uhuru wa vyombo vya habari, ni maendeleo dhahiri ya Tanzania. Ukumbatiwe.

## **SAFARI NA MAMA...**



**Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania, Deodatus Balile walipokuwa ndani ya ndege kuelekea Jiji la Ankara, Uturuki. Rais Samia na timu yake alikuwa na ziara rasmi nchini humo. Hii ilikuwa Aprili 17, 2024. (Picha na Ikulu)**

### **Jisajili kupata Pambazuko bure**

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### **NUKUU**



**Ni vyema na haki kwa kila mmoja wetu kukumbuka kujivua mzigo wa kiburi cha cheo au mali, na ajitwishe hisani, ubinadamu na tafakuri ya kujiweka katika viatu vya mwenzake. Hakika kiburi siyo maungwana na dhamana na mali huisha, lakini utu hudumu na kukumbukwa kwa mema daima - Abdulsamad Abdulrahim (mbobezi katika sekta ya nishati na madini Tanzania).**

## Tangazo

## Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,**  
**Oktoba, 2023**

## Changia Pambazuko liendelee

**WAJUMBE** wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukua Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hakuibaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata changamoto kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

**Tuma mchango wako kutoka mtandaoni wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263**

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandaa: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu



Lipa kwa kuscana



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI








## **TBS haitaki mchezo! Yaokoa maisha**

**Na Mwandishi WETU  
Dar es Salaam.**

**M**AISHA ya watumiaji wa bidhaa zinazoingizwa sokoni Tanzania, yako salama baada ya kuhakikishiwa na Shirika la Viwango (TBS).

Uhakikisho huo umekuwa ukitolewa kwa vitendo mara kwa mara na shirika hilo linapothibitika kuzuia matumizi na kuondoa sokoni kwa bidhaa zinazobainika kuwa na viwango hafifu na hata bandia.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, TBS imeteteza bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni sita ikiwa ni sehemu ya mikakati yake ya kuwalinda walaji nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dkt. Athuman Ngenya amesema bidhaa hizo zilikamatwa katika doria na ukaguzi unaofanywa na TBS katika soko.

“Lengo letu ni kuhakikisha kuwa tunamlinda mlaji dhidi ya bidhaa zenye viwango hafifu au bidhaa feki,” amesema.

Dkt. Ngenya amesema mkakati huo unahusisha pia kufanya tathmini ya usalama wa vyakula ambavyo vinazalishwa na kuuzwa kwenye masoko ya ndani na wajasiriamali.

Amesema vyakula vingi, ikiwamo mchele, maharage na mahindi ambavyo vinatumiwa na wananchi wengi, ndivyo vinalengwa katika tathmini hiyo.

“Tunajua kuwa watu wengi hununua vyakula katika maduka ya rejareja na wamiliki wa maduka hayo hununua vyakula hivyo moja kwa moja kutoka kwa wakulima, kwa kuwa inakuwa vigumu kufanya tathmini ya ubora wa vyakula vikiwa kwa wakulima huwa tunafanya tathmini hiyo kwa kukagua vyakula vilivyopo sokoni ili kuhakikisha kuwa walaji hawauziwi vyakula ambavyo ubora wake una mashaka,” amefanua.

Wakati huohuo, TBS imewaita wajasiriamali wazalishaji wa bidhaa, hasa vijana, kujitokeza kufanyiwa ukaguzi wa bidhaa zao ili wapatiwe vyeti na alama za ubora.

Dkt. Ngenya amesema kuwa



*Mkurugenzi Mkuu wa TBS,  
Dkt. Athuman Ngenya*

wajasiriamali hao wasihofu kuhusu gharama kwani Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fungu la fedha kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali hao kupata alama za ubora wa bidhaa zao kutoka TBS.

“Kwa hiyo wajasirimali wazalishaji watakaokuja na bidhaa zao kwa ajili ya ukaguzi, hawatatozwa kitu chochote kwani serikali ilitenga fungu na kulikabishi TBS kwa ajili ya kazi hiyo,” amefanua Dkt. Ngenya.

Amebainisha kuwa serikali imekuwa ikitenga kiasi cha shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuwawezesha wazalishaji wadogo nchini kupata leseni na alama za ubora wa bidhaa zao.

Utekelezaji wa majukumu

Hivi karibuni, Dkt. Ngenya aliwaambia waandishi wa habari kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita taasisi hiyo ilifanya vizuri katika utekelezaji wa kazi zake kiasi cha kupata mapato yaliyoiwezesha kutoa gawio kwa serikali.

“Katika kipindi hicho TBS imetoa gawio la jumla ya shilingi bilioni 18.1 kwa serikali. Tusingeweza kufanya hivyo kama ufanisi wetu ungekuwa ni wa chini,” ameegeza.

Dkt. Ngenya amesema kuwa hivi sasa TBS ipo katika mchakato wa ujenzi wa makao makuu mapya na maabara ya kisasa jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya kujiimarisha.

## Habari

## Serikali kupitia upya sheria za kamari

Na Mwandishi WETU

**S**ERIKALI imeahidi kupitia upya sheria inayohusu michezo ya kubahatisha (kamari) ili kuangalia vitendo hasi vinavyofanywa na waendeshaji wake ambavyo vinaweza kuhatarisha jamii.

Serikali imetoa msimamo huo kupitia kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande bungeni wiki iliyopita wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mlalo, Abdallah Shangazi (CCM).

Chande alionya kuwa wote wanaoendesha michezo hiyo kinyume cha sheria, serikali haitosita kuwachukulia hatua ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni zao.

Katika swali lake msingi, Shangazi alitaka kujua endapo serikali inatambua athari hasi kwa jamii ya Watanzania zinazotokana na ongezeko kubwa la michezo ya kubahatisha.

Pia katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alitaka kujua endapo serikali ipo tayari kupitia upya utoaji wa leseni kwa kampuni zinazoendesha michezo hiyo ambayo inachangia vijana, hususan wa kiume, kuathirika zaidi.

“Kwa kuwa michezo hiyo imethibitika inachangia ukatili wa kudhuru mwili, ukatili wa kingono, kiuchumi na kusababisha hata matatizo ya afya ya akili, je, serikali iko tayari kupitia upya utoaji leseni kwa kampuni hasa zile za mashineza bonanza ambazo zimetapakaa kote nchini?” alihoji mbunge huyo.

Katika majibu yake, serikali imekiri kuwa pamoja na kuwapo faida za kiuchumi na kijamii zinazotokana na michezo ya kubahatisha, zipo athari kwa jamii endapo michezo hiyo haitaendesha kwa weledi.

Naibu waziri huyo alitaja athari zinazoweza kujitokeza katika jamii kutokana na kamari, kuwa ni uraibu



*Naibu Waziri wa Fedha na Mipango,  
Hamad Hassan Chande*

pamoja na kugeuza kamari kuwa mbadala wa ajira.

Athari nyingine ni ushiriki wa watoto pamoja na kuwapo kwa michezo haramu isiyokuwa na usajili wa mamlaka.

Mjadala huo bungeni umetokea siku chache baada ya Pambazuko kuandika makala maalum kuhusu tishio jipya la changamoto ya afya ya akili kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na kampuni kutoka China katika Tanzania.

Habari hiyo maalum ilianguzia tafiti za wataalam wa tiba na tafiti za sayansi ambazo zimeonyesha kuwa uraibu wa kamari ni zaidi ya ule wa dawa za kulevya zikiwamo cocaine na heroin, huku Tanzania ikitajwa kuwa kinara wa waathirika wa michezo ya kamari kwa nchi zilizopo kusini mwa Jangwa la sahara.

Gazeti la Pambazuko limejitanabaisha kuwa kinara wa kufuatilia madhara ya michezo ya kamari na linaahidi kupambana hadi “kieleweke.”

## Matumizi ya mbegu za vinasaba kiama

Na Godwin CHILEWA,  
Texas, Marekani

**N**CHI nyingi masikini, hasa za Afrika, zinaaendelea kupokea misaada ya mbegu za mazao - zinazoitwa za kisasa, bila kuwa na njia za kitaalamu kutathmini madhara yake kwa ardhi, mazingira na viumbehai, hasa binadamu.

Mbegu hizo, hasa za mahindi, nyanya na mboga, zinatolewa kwa njia ya msaada na taasisi na kampuni kubwa na tajiri kutoka Marekani na Uingereza, huku zingine zikiletwa Afrika kwa ajili ya kufanyiwa majaribio.

Hata hivyo, imebainika kuwa nchi hizo masikini hazina vifaa vya kisasa wala watendaji wenye utaalamu na elimu kubwa kung'amua hasa madhara yake.

Mbegu zinazosambazwa kwa nchi masikini ni zile zilizobadilishwa vinasaba vyake na kupewa vipya, huzalishwa viwandani kutoka kwa matajiri, zinajulikana zaidi kwa jina na GMO (Genetically Modified Organism).

Pambazuko limebaini kuwa mbegu hizo hufika kwa nchi masikini kupitia miradi yenye fedha nyingi zinazotolewa na matajiri wa dunia kwa ajili kufanikisha malengo yao, mengi yakiwa na nia zilizojificha, hata kama itaeleza vinginevyo.

Mmoja wa miradi mikubwa ya kusambaza mbegu za mahindi zinazotajwa kuvumilia ukame ni ule unaiotwa Wema, ikiwani kifupi maneno ya Kiingereza - Water Efficient Maize for Africa.

Mradi huu ulianzishwa mwaka 2008, lakini ulipata nguvu zaidi kati ya mwaka 2013 - 2017. Mradi huo wenye ofisi zake jengo la Icraft House, Barabara ya Umoja wa Mataifa, eneo la Gigiri Village Market 00621, Nairobi, Kenya, unafadhiliwa na taasisi zinazoongozwa na matajiri zaidi duniani ni pamoja na Bill and Melinda Gates, Howard and Buffet, pamoja na Agency for International Development



*Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe*

(AID), zote za Marekani.

Lengo la wazi la mradi huu unaeleza kuwa ni kuzisaidia nchi maskini kuzalisha mahindi zaidi ili kujitoshesha kwa chakula. Tofauti na miradi mingine ya kilimo cha kawaida, mradi huu unahimiza matumizi ya njia za kitaalamu (Bleeding - Biotechnology) kuzalisha mahindi ya GMO.

Wataalamu wa mradi huo wanadai kuwa mkulima anayetumia mbegu na utaalamu wa kupanda na kutunza mbegu hizo, anaweza kupata ongezeko la mavuno kuanzia asilimia 24 hadi 35 zaidi, kulinganisha na “ukulima wa kawaida” - asiyetumia mbegu hizo.

Hadi sasa, mradi huo wa Wema, unaaendelea kufanya utafiti wa mbegu zinazotajwa kuwa bora zinazohimili ukame, kufanya makongamano ya kutoa elimu na kuhimiza matumizi ya mbegu za kisasa pamoja na viwatilifu vinavyokwenda sambamba.

Mradi huo pia unafanya jitihada za kuwawezesha wakulima wadogo kupata masoko ya mazao yao, kujipana kwa kuongeza uzalishaji kwa kila hekari, kazi hizo hufanywa pia kwa kushirikiana na asasi nyingine.

Uchunguzi umebaini kuwa mikakati ya mradi huo na mingine inayofadhiliwa na nchi tajiri, ikitazamwa kwa haraka-

## Habari

## Matumizi ya mbegu za vinasaba kiama

*Inatoka Uk. 7*

haraka, wengi wanaweza kuamini kwa asilimia 100 kuwa ni mizuri na yenye tija kubwa, lakini baadhi ya watu waliohojiwa na Pambazuko wanadai miradi hiyo ya mbegu za GMO, inalenga kuzitumbukiza nchi za Afrika kwenye utegemezi wa mbegu na viuatilifu kutoka nje, na kuacha “utamaduni uliozoeleka miaka mingi” wa kuhifadhi mbegu kwa kila msimu wa mavuno.

Mbali na kuwa na utegemezi wa mbegu, pia matajiri huenda wana malengo yaliyojificha ili kuhakikisha Waafrika wanaendelea kuwa tegemezi kwa mbegu na hata kujitegemea kwenye ulaji wa vyakula vilivyotengenezwa kwa GMO,” anaoneza Dkt. Kija Matuja, mtaalamu wa Kilimo anayeishi Ngudu, Kwimba Mwanza, alipohojiwa na Pambazuko.

Kawaida - tangu enzi na enzi, suala la kutunza mbegu lilikuwa la kila familia, lakini baadaye serikali za nchi nyingi Afrika, ikiwamo Tanzania, zilianza kugawa mbegu za baadhi ya mazao na kutoa ushauri wa kitaalamu namna ya kuzitunza gharani na shambani baada ya kupandwa. Hizi hazikuwa zimebadilishwa vinasaba.

Pambazuko limezungumza na baadhi ya wataalamu wa kilimo ambao wameeleza kuwa mbegu za GMO, hununuliwa kwa kila msimu na haziwezi kutunzwa baada ya mavuno kama ilivyokuwa kwa mazao ya asili.

“Mbegu zinazopigiwa chapuo na matajiri, wanaoitwa wafadhili, haziwezi kutunzwa wala kuhifadhiwa kutoka kwenye mazao ya GMO, lazima kila mwaka mkulima anunue, huu ni utumwa mwingine unaoletwa kwa nchi masikini,” amesema Josephat ole Kise, aliyejitambuisha kwa Pambazuko kuwa ni mkulima wa kawaida anayeishi Handeni, Tanga.

Kimsingi kilimo cha mazao ya GMO ndicho kilichowezesha nchi zilizoendelea,



*Mbegu za GMO*

ikiwamo Marekani na Uingereza kudhibiti uzalishaji na matumizi ya vyakula nchini mwao. Mtu anayeishi katika nchi hizo akitaka kulima bustani analazimika kununua mbegu, viuatilifu, na hata udongo wa kupandia mimea anayoitaka kutoka kwa wauzaji wakubwa.

Hatua hii imewafanya wananchi wa kawaida kuwa wanunuzi wa vyakula na hata mboga ambazo wangeweza kujipanda wenyewe huku wakulima matajiri (makabaila) wakiendelea kuwa na soko la uhakika wa mazao yao.

Imebainika kuwa mazao yanayozalishwa kwa mbegu za GMO hupoteza ubora wa kuwa na mbegu zinazoweza kuhifadhiwa kwa msimu ujaar, ndiyo maana hata ubora wa mazao lishe yanayopatikana ni duni ikilinganishwa na mazao yaliyozalishwa kwa mbegu halizi-zinazoweza kuitwa “za kienyeji.”

Ndiyo maana hata mazao yanayopatikana kutokana na mbegu za GMO, hulazimisha kuongezwa kuongeza virutubisho kwenye ili kukidhi haja ya mahitaji ya mwili.

Katika suala la kiusalama, Pambazuko limespokezwa kuwa vyakula vya GMO vinaweza kutumika kama silaha za maangamizi, kwani wakati wa uzalishaji wa mbegu zake wataalam wanaweza kutumia teknolojia ya kisasa inayoitwa NRA effect technology, kupandikiza vimelea vya sumu au vinavyoweza kubadilisha vinasaba vya mlaji kwa namna wanayotaka.





## Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

### Tutaonea haya wabadhirifu mpaka lini?

**M**WISHONI mwa Machi, 2024 Rais Samia Suluhu Hassan alikabidhiwa ripoti mbili zilizoibua 'madudu' kwenye mashirika ya umma na zilionyesha jinsi baadhi ya watendaji walivyoshiriki kutia hasara nchi.

Ripoti hizo ni ile ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichele ya mwaka 2022/2023 iliyoonyesha baadhi ya mashirika ya umma yanayojiendesha kibiasara yalivyopata hasara ya mabilioni ya shilingi na kuongezeka deni la serikali.

Nyingine ni ile ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Salum Hamduni, ambayo iliweka hadharani namna baadhi ya watendaji serikalini walivyojimegea mafungu ya fedha za miradi ya maendeleo, huku miradi hiyo ikiwa haijatekelezwa!

Kwa ujumla, kupitia ripoti zote mbili zilikabidhiwa kwa Rais Samia, tulijionea jinsi safari hewa zilivyoondoka na shilingi bilioni 1.3, huku ikibainishwa shilingi bilioni 12 zilizokusanywa katika Jiji la Dar es Salaam na kutokomea kusikojulikana, ingawa "karatasi" zilionekana zimepeleka benki.

Aidha, tuliona Kampuni ya Simu (TTCL), Shirika la Reli Tanzania (TRC), Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) yalivyobainika kupoteza mabilioni ya shilingi.

Pia ubadhirifu wa takriban shilingi bilioni 14 kwenye Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam (UDA) uliofanywa na iliyokuwa menejimenti ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART).

Hizi ni fedha nyingi sana zilizohibitika kukwapuliwa ama kuchepushwa na CAG, lakini inashangaza kwamba wapo viongozi wanaosema - 'hakuna senti hata moja ya serikali inayoibwa.'

Kauli hiyo ya kutetea inakatisha tama na inajenga hisia kuwa anayeitoa ana



Salum Hamduni

Watanzania kuwa mazuzu!

Kitu cha kushangaza ni kwamba, pamoja na ripoti hizi mbili kufanyiwa kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote, na hatimaye kuwasilishwa kwa rais, siyo ajabu baadaye tutaambiwa Takukuru imeshindwa kuwafikisha mahakamani wahusika kwa kukosa ushahidi! Tukifanya hivyo itakuwa sawasawa na 'kufuga' jipu lililowiva!

Ni muda mrefu sasa nchi yetu imestawisha utamaduni wa mtendaji wa serikali au shirika la umma anapoharibu ama kushindwa kutekeleza vyema majukumu yake, uhamishwa na kupeleka kituo kingine cha kazi, kama vile kule anakopeleka ndiko waliko watu wasiohitaji uchapakazi uliotukuka. Tuuzike utamaduni huu, la sivyo tunapalilia uzembe!

Hivi nani aliyeturoga na kutudanganya kwamba, mtendaji akishindwa kuwajibika kwenye majukumu yake, dawa yake ni kumuhamisha na kumpeleka kituo kingine

Hivi ukiambiwa kwenye ripoti ya Kamishna Hamduni kuna shirika moja la umma limeitia hasara serikali kwa kufanya ubadhirifu wa mabilioni ya shilingi ya Watanzania, halafu bosi aliyekuwepo kwenye shirika hilo wakati hasara hiyo inatokea, sasa hivi amepandishwa cheo yuko wizarani, utaamini?

Mwandishi anapatikana kwa simu namba 0784 438546

Barua pepe:mtagaluka@gmail.com

**Kenya****Mbinu ya Rais Ruto kumaliza mafisadi**

NA Julius MKAMBI,  
Nairobi

**S**AKATA la mbolea ghushi nchini Kenya limeitikisa serikali ya Rais William Ruto ikizingatiwa moja ya ajenda zake kuu wakati wa kampeni ilikuwa kuboresha sekta ya kilimo na kutoa ahadi kwa wakulima kuwapa mbolea ya bei nafuu.

Hata hivyo, kwa siku za hivi karibuni, wakulima kutoka maeneo ambayo shughuli kubwa kilimo, wamekuwa wakilalamika kuuziwa mbolea ghushi zenye nembro ya Bodi ya Taifa ya Nafaka na Mazao (NCPB).

Licha ya kilio hicho, Waziri wa Kilimo, Minthika Linturi, mara kadhaa amekana taarifa hizo akisisitiza kuwa anasubiri uthibitisho kutoka kwa Shirika la Viwango Kenya (KeBS, kauli ambayo imewakera Wakenya wengi, huku wabunge wakimtaka Rais Ruto kumtimua kazi kutokana na “utepetevu kazini.”

Baada ya kimya kirefu, Rais Ruto alitoa msimamo wake, huku akihusisha usambazaji wa mbolea hiyo na ufisadi. Alisema wale wote wanaohusika na usambazaji wa mbolea ghushi kurudisha fedha kwa wakulima waliowauzia na kuamuru kukamatwa kwa wahusika.

Rais Ruto alirudia kauli yake aliyoitoa mwishoni mwa mwaka jana ya ‘mambo matatu,’ ikiwa ni onyo kali kwa mafisadi na wafujaji wa mali ya umma.

Japo ni kauli iliyopingwa na wanasiasa kutoka mrengo wa upinzani, Chama cha Sheria Kenya na baadhi ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, wapo wanaohisi muda sasa umefika kuona Rais Ruto akitekeleza kwa vitendo ‘mambo matatu’ kwa nia njema ya kuwakomesha mafisadi.

Kiongozi huyo wa nchi alisema matamshi yake hayo hayakuwa ya mzaha na kwamba hivi karibuni, watu wataanza kuona akiyatekeleza kwa vitendo ikiwa ni msisitizo ya adhabu inayowasubiri wabadhirifu wa mali ya umma.

“Hivi karibuni mtaanza kuona namna



*Rais wa Kenya, William Ruto*

tutakavyowashughulikia wale wote wanaohusika kuiba na kuharibu mali ya umma, nyinyi wote mnajua mambo yao ni matatu,” alisisitiza Ruto hata ingawa huenda aliyatoa kwa utani.

Mambo hayo matatu ambayo Rais Ruto anawaambia mafisadi kuchagua ni; kuhama Kenya, kwenda jela au kusafirishwa kwenda mbinguni.

Hilo la ‘kusafirishwa kwenda mbinguni’ ndilo lililobeba tafsiri pana likihusishwa na kuwaangamiza wanaotafuna mali ya umma, hivyo kukosolewa zaidi, huku wakosoaji wakimtaka Ruto kutathmini matamshi yake.

Seneta wa Kilifi ambaye pia ni kiongozi wa upinzani kwenye Bunge la Seneti, Stewart Madzayo, alisema “matokeo mabaya” ya matamshi ya mkuu wa nchi hayawezi kupuuzwa.

“Sisi, Azimio la Umoja (muungano wa vyama vya upinzani), tunalaani matamshi kama haya yaliyotolewa na Rais Ruto kwa vile hii ni nchi ya kidemokrasia inayoongozwa na utawala wa sheria, na athari mbaya za kauli kama hizo haziwezi kupuuzwa,” Madzayo alisema.

Hata hivyo, Kiongozi wa Wengi Bunge la Taifa, Kimani Ichung’wah, ametetea kauli ya ‘mambo matatu’ ya Rais Ruto akisema hiyo ni njia bora ya kukabiliana na ufisadi.

## Rais Samia anateua wasaidizi asioamini?

Na Elphaz CHARLES

**M**ARA kwa mara tumekuwa tukishuhudia Rais Samia Suluhu Hassan akifanya mabadiliko na uteuzi wa mawaziri, wakuu wa mikoa, wilaya, wakuu wa vitengo na taasisi za umma sanjari na mabalozi.

Kimsingi, lengo la mabadiliko na uteuzi ni kuongeza nguvu na ari ya kiutendaji kwa viongozi ambao miongoni mwao wamekuwa na kasumba ya kuyazoea madaraka, huku wakisahau kuwa cheo ni sawa na koti la kuazima, hivyo muda wote unaweza kunyang'anywa.

Hata hivyo, katika uongozi wa Rais Samia, wapo baadhi ya viongozi wanaonekana kuwa wameshindwa mahali fulani kutokana na sababu mbalimbali kama uzembe, matumizi mabaya ya ofisi, na matumizi mabaya ya rasilimali za taifa, lakini bado wanaonekana wamo kwenye mabadiliko yanayotangazwa, huku wakibadilishwa-badilishwa.

Kuna nyakati mtu anaweza kutilia shaka utashi wa viongozi hao pamoja na wasimamizi wao kutokana na uzembe ambao husababisha kupotea kwa mabilioni ya fedha ambazo ni mali ya wananchi pamoja na mikopo ambayo huzaa deni la taifa.

Siku hizi majina ya mawaziri na wakuu mbalimbali yanabadilika kila mara, hii inadhirisha kuwa huenda Rais Samia hajapata viongozi sahihi wa kuendana na matamano, pamoja na kasi ya utendaji wake.

Watanania wamekuwa wakishuhudia aliyemteua miezi mitatu iliyopita, Rais Samia akimtoa au kumbadilishia kitengo na wengine hubadilishwa saa chache tu baada ya kuwateua, yaani wanatenguliwa hata kabla ya kuapishwa.

Inavyoonekana hata wale waliopata dhamana, bado wapo baadhi wanaomwangusha mteuzi kwa kutojituma, kuwa wabunifu na wengine woga tu wa kuchukua hatua, wakisubiri kiongozi wa nchi kufanya kila jambo au



*Rais Samia Suluhu Hassan*

kutoa kauli, hata kama wao wanaweza.

Kuna nyakati Rais Samia anajaribu kuwaelekeza mambo kadhaa na kuwakumbusha majukumu yao, lakini matokeo yake hayaonekani kabisa, yaani kwa maneno mengine ni kuwa kiongozi huyo wa nchi anapambana kunyoosha vivuli kwa kuendelea kuwapa imani wasioaminika.

Kwa sababu kuna viongozi ambao uwezo wao umekuwa mdogo na wameshindwa wizara au vitengo fulani, lakini bado wanaendelea kubadilishiwa wizara badala ya kuondolewa ili wapatiwe majukumu hayo wale wanaoyaweza kuliko kuendelea kuwapa imani.

Tanzania ina zaidi ya watu milioni 60 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Agosti, 2022, kwa mantiki hiyo ni wazi katika idadi hiyo hatuwezi kukosa Watanzania milioni 20 wenye uwezo wa kuongoza kuliko kuwang'ang'ania viongozi haohao.

Ifahamike kuwa katika nchi yenye uongozi bora, na wenye uwezo wa kutenda, umasikini ni kitu cha kuonea haya, kwani wao ndiyo chachu kubwa ya maendeleo kwa jamii, hivyo tukiona hakuna maendeleo yanayotarajiwa, moja ya sababu ni kuwa na viongozi wabovu.

*Mwandishi ni msomaji wa Pambazuko na abapatikana kwa simu: 0685 872 763 na Email: elphazcharles@gmail.com*

## Habari

## Bandari Tanga yazaliwa upya

Na Mwandishi WETU,  
Tanga

**U**CHUMI wa Jiji la Tanga sasa unatazamiwa kukua na pia kuwepo neema ya makusanyo zaidi ya kodi Tanzania, baada ya kufanyika kwa maboresho makubwa katika Bandari ya Tanga.

Maboresho hayo yaliyofanywa kupitia awamu mbili za uwekezaji, yameiwezesha bandari hiyo kuanza kuvutia wateja wa kimataifa.

Akizungumza na waandishi wa Pambazuko walioambatana na wahariri wa vyombo vingine kutembelea bandari hiyo mwishoni mwa wiki, Meneja wa Bandari ya Tanga, Masoud Mrisha, alisema shehena inayosafirishwa kupitia bandari hiyo imeongezeka katika kipindi cha miaka ya karibuni sambamba na ongezeko la mapato.

Amesema idadi ya wafanyabiashara wa nje ya Tanzania wanaotumia bandari hiyo, imeanza kuongezeka kama ilivyo yote inakwenda Jamhuri ya Kidemokrasia na Congo yaani DRC. Shehena ya shaba inayosafirishwa kupitia bandari yetu nayo imeanza kuongezeka," alisema.

"Ile meli mnayoiona pale (akiisonta), inapakua shehena ya sulphur ambayo yote inakwenda Jamhuri ya Kidemokrasia na Congo yaani DRC. Shehena ya shaba inayosafirishwa kupitia bandari yetu nayo imeanza kuongezeka," alisema.

Meneja Mrisha pia alisema baada ya maboresho sasa bandari hiyo imerekodi ongezeko la wafanyabiashara kutoka nje ya nchi ambao wameifanya kuwa mahsusi kupitisha mizigo yao.

Uwekezaji huo wa jumla ya Shilingi bilioni 429.1 uliofanyika kwa awamu mbili umeboresha miundombinu na kuongeza vifaa vinavyotumika bandarini hapo, hivyo kuongeza ufanisi.

Pia uwekezaji huo umefanikisha upanuzi wa gati za kupokea meli, ununuzi wa vifaa vya kushughulikia shehena, kuongeza kina na upana wa mlango wa bahari, kuongeza kina cha eneo la kugeuzia meli na pia maboresho



*Meneja wa Bandari ya Tanga, Masoud Mrisha,*

mengine ambayo yameifanya bandari hiyo kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuhudumia meli.

Pambazuko linatambua kuwa awamu ya kwanza ya uwekezaji huo ilianza mwaka 2019 ikigharimu kiasi cha Shilingi bilioni 172.3 zilizotumika kuongeza kina kwenye mlango wa bahari kutoka meta tatu hadi meta 13 na upana wa meta 73.

Zamani meli iliyokuwa na kina cha zaidi ya meta tatu ilikuwa haiwezi kuingia bandarini hapa moja kwa moja. Meli zilikuwa zinapaki mbali na bandari, kama kilometa 1.7 hivi na mizigo ilikuwa inapakuliwa kwenye matishari ambayo ndiyo yalikuwa yanafikisha mizigo bandarini.

Imefahamika kuwa kazi ya kupakua na kupakua shehena ilikuwa inafanyika mara mbili; kwanza kupakua kutoka kwenye meli na kuingiza mizigo kwenye matishari na kisha kupakua kutoka kwenye matishari kuishusha mizigo bandarini.

Mrisha alieleza kuwa hatua hiyo hiyo liliongeza gharama kwa wasafirishaji na pia kuzifanya meli kukaa muda mrefu hapa.

"Lakini baada ya maboresho bandari sasa ina uwezo wa kupokea meli yenye kina cha hadi meta 12 na mlango unaruhusu meli yenye upana wowote kuingia bandarini moja kwa moja bila

## Bandari Tanga yazaliwa upya

**Inatoka Uk. 12**

kikwazo,” alisema Mrisha.

Aidha, awamu hiyo ya maboresho ilihusisha pia ununuzi wa vifaa vya kisasa 16 vikiwamo ‘Crane’ mbili ambayo kila moja ina uwezo wa kubeba tani 100 za shehena kwa wakati mmoja, magari ya kubebea mizigo ndani ya bandari, mitambo mitano ya kuinua mizigo yenye uzito mbalimbali, ‘rubber tire gantry’ na vifaa vingine.

Katika awamu ya pili, shilingi bilioni 256.8 zilitumika kuboresha gati mbili bandarini hapo kwa kuongeza kina cha bahari kutoka meta tatu hadi meta 13 na pia kupanua gati kwa meta 50 kwa upande mmoja na meta 90 kwa upande wa pili.

“Kwa ujumla uwezo wa bandari kuhudumia shehena umeongezeka na kufikia kikomo cha tani milioni tatu kwa mwaka. Pia tumepunguza gharama, kwani meli sasa zinatia nanga bandarini moja kwa moja na hatutumii tena matishari kupakua mzigo kwenye meli,” alisema.

Ni kutokana na hatua hiyo, muda wa meli kukaa bandarini hapo umepunguzwa kutoka wastani wa siku tano zamani hadi wastani wa siku mbili hivi sasa kutokana na kuongezeka kwa ufanisi na utendaji kazi.

“Idadi ya meli kubwa zinazofika bandarini hapa zimeongezeka pia, sasa tumeanza pia kuvutia shehena ya

shaba kutoka Zambia na hadi hivi sasa tumeshasafirisha zaidi ya tani 9,000 za shaba kupitia bandari yetu hii,” alisema Mrisha.

Mrisha alisema katika kipindi cha miaka mitano, shehena inayohudumiwa bandarini hapo imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 12.2 kwa mwaka, huku idadi ya meli zinazohudumiwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 16.2 kwa mwaka.

Tanga ndiyo bandari kongwe hapa nchini. Ilijengwa na wakoloni wa Kijerumani katika miaka ya 1880 na wakati huo ikijulikana kwa jina na ‘Marine Jet.’

Maboresho ya zamani yaliwezesha gati la kwanza kwenye bandari hiyo kujengwa mwaka 1915, likiwa na urefu wa meta 221, huku gati la pili lenye urefu wa meta 229 likijengwa mwaka 1954.

Hivi sasa Bandari ya Tanga ina eneo lenye ukubwa wa hekta 17 ikiwa inahudumia pia bandari nyingine ndogone za Kipumbwi, Pangani, Mkwaya na Sahare.

Pia kuna eneo la Mwambani lenye ukubwa wa hekta 176 na Chongoleani lenye ukubwa wa hekta 207 ambayo sehemu yake imekabidhiwa kwa serikali kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya kusafirisha mafuta ghafi yatakayosafirishwa kutoka Uganda kwenye mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (Eacop).



Meli kubwa ikiwa imetia nanga Bandari ya Tanga. Picha ilipigwa na Mpigapicha wa Pambazuko Aprili 19, 2024

## Habari

## Matumizi ya mbegu za vinasaba kiama

*Inatoka Uk. 7*

Hii ina maana kuwa wanaweza kupandikiza vimelea vya kusababisha kansa, kupunguza nguvu za kiume, kuharibu mimba, au kuchochea tabia zisizoendana na maumbile ya mhusika – mwanamke anaonekana mwanaume na kinyume chake.

Pamoja na kwamba nchi tajiri zinahimiza nchi masikini kutumia GMO, zenyewe zinawaasa wananchi wake kula vyakula vilivyozalishwa kwa mbegu asili na bila mbolea za kemikali wala dawa za kuua wadudu (Organic Food) kwa afya na usalama wa miili yao.

Wakati nchi nyingi za Afrika, Tanzania ikiwamo, zinaendelea kusuasua kujipanga na kulinda watu wao, hivi karibuni Marekani imeridhia kuwalipa fidia watu waliopata madhara (kuugua kansa) kufuatia majaribio ya bomu la Atomic (Manhattan Project Trinity test) yaliyofanyika New Mexico Julai 16, 1945.

Vizazi vya wahanga hao wameahidiwa kulipwa mamilioni ya dola kwa sababu serikali imekiri kwamba ilifanya makosa. Hii inaonesha jinsi wenzetu wanavyojali thamani ya utu, wanavyotunza kumbukumbu, na walivyo tayari kusimamia haki zao kizazi na kizazi. Aidha kwa funzo hilo wenzetu wamefanya mabadiliko makubwa kwenye mifumo ya uendeshaji wa mambo yao hasa namna ya kulinda afya na usalama wa watu wao. Hawa ndio watu ambao tunawaita mabepari na mabeberu.

Uchunguzi uliufanywa na mwandishi umebainisha kwamba wasimamizi wa miradi mingi nchini hufanya jitihada kubwa kufanikisha miradi yao ili kujipatia heshima, na kuendelea kupokea fedha za wafadhili, lakini hawawezi kipaumbele kwenye masuala ya usalama wa taifa.

Hii ni kwa sababu wanaopewa nafasi za kuwa waangalizi hulipwa fedha nyingi na wafadhili kati ya shilingi 250,000 na 400,000 kwa siku, ikilinganishwa na shilingi 100,000 hadi 150,000 kwa



*Mbegu za GMO*

siku zinazotolewa na serikali kwa kazi hiyohiyo.

Hili ndilo linalosababisha miradi hatari iendelee kufanyika nchini Tanzania kwa uhuru kwani hakuna anayethubutu kuilalamikia.

Katika nchi nyingine majaribio ya kisayansi husimamiwa kwa ukaribu na idara za usalama wa taifa za nchi husika kupitia idara na vitengo vya kificho vilivyojipenyeza au kuundwa maalum kwa lengo hilo. Hili ndilo linaloweza majaribio hayo kufanywa kwa ufanisi, usiri wa hali ya juu, na kwa usalama zaidi.

Tanzania inazo asasi zisizo za kiserikali zenye malengo na mwelekeo mzuri, tatizo ni kuwa asasi hizo pia zinaendeshwa kwa misaada ya wafadhili jambo linalozipunguzia nguvu ya kufanya kazi. Baadhi ya asasi hizo ni Tanzania Alliance for Biodiversity (Tabio) African Center for Biodiversity (ACB) na Tanzania Organic Agriculture Movement (Toam).

Ikumbukwe kuwa Novemba 21, 2018, Tanzania ilipiga marufuku majaribio ya mbegu za GMO kupitia kauli ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mathew Mtigumwe ambaye aliagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) kusitisha mara moja utafiti na majaribio ya mbegu hizo. Aliamuru pia kuteketezwa kwa mabaki yote ya majaribio hayo.



# *Tangaza na* **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au  
Barua- Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

## Uchambuzi

### Muungano utaimarika kwa kuunganisha watu

Na Mwandishi WETU

**I**JUMAA ya wiki hii, miaka 60 inatimia kwa jambo kubwa kufanyika Aprili 26; la nchi mbili kuungana na kuzaliwa nchi moja.

Hata hivyo, pamoja na umri huo kuwa mkubwa, ni jambo la kusikitisha kuwa miaka 60 baada ya iliyokuwa Tanganyika kuungana na Zanzibar na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mazungumzo kuhusu Muungano huo yamejikita zaidi kuhusu kero.

Viongozi wanatuambia kuwa kuna faida nyingi sana za Muungano zilizopatikana, ingawa kuna kero chache sana ambazo zinashughulikiwa.

Kauli hizi za viongozi ni kweli, lakini ukiona kero chache zilizosalia ndizo zinakuwa gumzo dhidi ya faida nyingi zilizopatikana katika Muungano, ni dhahiri kuwa kero hizo, pamoja na uchache wake, zinazidi uzito wa mafanikio yaliyopatikana, pamoja na wingi wake.

Kingine kinachosikitisha zaidi ni kuona kuwa miaka 60 baada ya kuungana, bado tunazungumzia kero na jinsi ya kuzitatua badala ya mijadala kujikita kwenye uimarishaji wa Muungano huo.

Ni kweli, tuliungana tukiwa hatujajiandaa vya kutosha kama nchi. Wakati Muungano unafanyika wananchi wengi hawakuwa wameelimishwa kuhusu Muungano huo, hivyo kuwa na uelewa finyu kuhusu.

Lakini, ilitarajiwa kuwa baada ya miaka 60, kasoro na matatizo yote yaliyotokana na kutojiandaa vyema kabla ya kuungana, viwe vimeshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi.

Miaka 60 ni mingi sana kwa mtu mwenye dhamira ya kweli kufanya jambo fulani na kukamilika, lakini inaonekana Tanganyika na Zanzibar, hazikuwa na dhamira hiyo au labda kulikuwa na jambo lililosukuma kutokea kwa muungano huo, ambalo halizungumzwi. Iweje miaka 60, bado tunazungumzia kero?



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania- Samia Suluhu Hassan*

Kama tumeshindwa kumaliza kero za Muungano katika kipindi cha miaka 60, hivi tutahitaji miaka mingapi zaidi kumaliza kero hizo?

Tukumbuke kuwa nyingi ya kero hizi zilizaliwa pamoja na Muungano, lakini hadi hii leo bado zipo. Hii ina maana kuwa Muungano unazeeka na kero zake zinazeeka pia! Zipo.

Ni kweli kuwa Muungano una faida kubwa kwa nchi na wananchi wake. Lakini uwepo wa kero hizi unadhoofisha sana faida za Muungano huo na kuufanya uonekane kutokuwa na maana kwa baadhi ya watu.

Hii ni kwa sababu inavyoonekana, Muungano bado ni kero, ndiyo maana muda mwingi unatumika kuzungumzia na kushughulikia kero na siyo kufaidi matunda yake.

Hatuwezi kujivuna kuwa tumefaidi Muungano wakati hadi leo bado hata muundo wa Muungano wenyewe, hili nalo ni suala linaloendelea kubishaniwa.

Ingekuwa suala hilo linabishaniwa na upande mmoja wa Muungano, labda tungenema kuwa ni kutokana na ubinafsi, lakini malalamiko kuhusu muundo wa Muungano yanatoka pande zote za nchi husika.

Wakati Watanganyika wakihoji kwa nini serikali yao ife na kumezwa ndani



## Muungano utaimarika kwa kuunganisha watu

*Inatoka Uk. 16*

ya Muunganpo, Wazanzibari bado hawaridhiki na nafasi ambayo serikali/nchi yao imepewa ndani ya Muungano.

Wakati Watanganyika wakiamini kuwa licha ya serikali yao kumezwa yote ndani ya Muungano, lakini hawajapatiwa nafasi ya kutosha ndani ya Muungano huo kutoka na upande wa pili kulinda maslahi yake na kuweka taratibu za kisheria zinazowatenga Watanganyika wanaotaka kutekeleza matakwa ya Muungano ya kwenda na kuishi popote.

Kwa upande wao Wazanzibari, ingawa wana uhuru wa kwenda na kuishi popote, bado wanaamini kuwa serikali na mamlaka ya nchi yao yamemezwa ndani ya Muungano na kuiacha serikali yao ikiwa dhaifu.

Kuna migogoro pia kuhusu mgawanyo wa mapato na uwakilishi kupitia Muungano.

Hapa Wazanzibari wanakumbusha kuwa kabla ya Muungano, Zanzibar ilikuwa na kiti Umoja wa Mataifa, lakini ndani ya Muungano, Zanzibar inatakiwa kupata ruhusa ya Jamhuri ya Muungano hata pale inapotaka kujiunga na jumla za kimataifa huku suala la kuwa na balozi likifutika kabisa.

Lakini, lipo pia suala la mgawanyo wa mapato na rasilimali. Mpaka leo hii bado Watanganyika wanahoji kuhusu mchango wa Zanzibar katika uendeshaji wa Serikali ya Muungano.

Inafahamika kuwa hakuna mchango wa moja wa moja kutoka Serikali ya Zanzibar katika Bajeti Kuu ya Serikali ya Muungano, ingawa ipo baadhi ya miradi inayotekelezwa kupitia bajeti hiyo ambayo inachangiwa kwa asilimia kubwa na Serikali ya Muungano inanufaisha pia Zanzibar na watu wake.

Watanganyika wanahoji kwa nini mapato ya gesi na madini yanayochimbwa katika eneo la iliyokuwa Tanganyika, yanainufaisha pia Zanzibar, wakati kwa utaratibu uliopo sasa gesi, mafuta au madini yanakayopatikana katika eneo



*Rais wa Zanzibar - Dkt. Hussein Ali Mwinyi*

la Zanzibar - yakiingiza mapato, yote yanakwenda kwa Serikali ya Zanzibar pekee?

Shughuli za kiuchumi zinazofanywa na Serikali ya Muungano zinainufaisha pia Zanzibar, wakati shughuli za kiuchumi zinazofanywa na Zanzibar, ni kwa manufaa yake pekee, bila kuhusisha mshirika wake wa Muungano.

Kwa ufupi, wakati Zanzibar ikibakia na mamlaka fulani kiuchumi, kisiasa na kijamii ndani ya Muungano, mamlaka hayo yameondoka kabisa kwa Tanganyika ambayo imemezwa jumla jumla na Muungano.

Tumeshuhudia kwa miaka mingi kero hizi zikipatiwa nguvu sana kutokana na tofauti za kisiasa zilizopo. Wakati Watanganyika wanajiona kuwa wao ndio wenye eneo kubwa zaidi kijiografia ndani ya Muungano, lakini wanashangaa kuwa idadi ya viongozi wa kisiasa ndani ya Serikali ya Muungano kutoka Zanzibar, haina uwiano na ukubwa wa eneo hilo kijiografia.

Wazanzibari nao wana malalamiko ya muda mrefu kuwa mfumo wa kisiasa uliowekwa unasababisha watu wa Tanganyika kwamua hatma ya nani awe kiongozi wa visiwa hivyo.

Hivi karibuni tulishuhudia mjadala mkali kwa watu wa jamii ya Kimasai wakiingia katika msugvano na mamlaka za ulinzi visiwani Zanzibar. Baada ya

## Uchambuzi

### Muungano utaimarika kwa kuunganisha watu

*Inatoka Uk. 17*

hapo ukaibuka mjadala mwingine kuhusu watu waliopewa adhabu bila kufuata utaratibu kwa tuhuma za kula hadharani wakati wa Mwezi wa Ramadhan.

Wakati hayo yakiwa yanatokea upande wa Zanzibar, hakuna matukio ya mtu kunyanyaswa kwa namna yoyote ile upande wa Tanganyika kwa maelezo tu kuwa amekiuka utamaduni wa eneo husika na kwa sababu yeye ni Mzanzibari kama vile tulivyoshuhudia kwenye video ya wale walioadhibiwa kwa kula mchaka wakitajwa kuwa ni watu wa Tanganyika.

Kwa muda mrefu sana kumekuwa na madai ya kuandikwa kwa katiba mpya itakayokuwa na vipengele vya kuuimarisha Muungano, lakini madai hayo bado hayajatekelezwa.

Serikali ya awamu ya nne, ikiiongozwa na Rais Jakaya Kikwete, ilianzisha mchakato wa kuandika katiba mpya, lakini kati ya mambo yaliyozua msugungano mkubwa ni muundo wa Muungano.

Kwa kuwa kutafuta ufumbuzi wa masuala ya Muungano kwa njia ya kisiasa inaonekana kama mfupa mgumu,

ni vyema sasa tukafikiria nje ya boksi na kuwa na utaratibu mwingine wa kuimarisha Muungano wetu.

Uzoefu unaonyesha kuwa pale ambapo watu, kwa nafsi zao, wanapokubaliana jambo katika ngazi ya nafsi zao, basi mara nyingi jambo hilo hufanikiwa.

Kwa kuwa tunalifahamu hilo, nadhani ni wakati sasa wa kufikiria namna ya kuwaunganisha watu wa pande hizi mbili na kuwafanya wajione kuwa wamoja zaidi.

Kwa jinsi hali inavyoonekana, kumekuwa na msugungano baina ya watu wa pande hizi mbili za Muungano kwa sababu tuliunganisha nchi tukacha kuwaunganisha watu wa nchi hizo.

Matokeio yake, Muungano umebaki zaidi kuwa wa vitu na maneno zaidi kuliko wa nafsi na vitendo.

Uhalisia ni kuwa Muungano unasemwa zaidi kuliko kutekelezwa. Iwapo tutataka Muungano utekelezwe zaidi, basi juhudi zinatakiwa kufanyika ili kuwaunganisha watu badala ya serikali au nchi.

Watu wakiamua kuungana hawataziona tena tofauti zao, kwani

w a t a j i o n a  
kuwa wamoja  
zaidi. Lakini  
t u k i e n d e l e a  
kufanya siasa,  
r a s i l i m a l i,  
maeneo ya  
kijiografia kama  
ndio msingi  
wa Muungano  
siku,  
tutashuhudia  
mitafaruku kwa  
sababu watu  
w a n a o m i l i k i  
hayo, bado  
katika mioyo  
yao wana  
u b i n a f s i  
wa mali na  
rasilimali zao.



Rais wa Tanganyika, Mwalimu Julius Nyerere (kushoto), akiweka saini hati ya Muungano, kama ambavyo pia anafanya Rais wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume. Wanaoshuhudia ni baadhi ya viongozi waandamizi wa nchi hizo mbili. (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko).

## Elimu ya mafao kinga dhidi ya 'majanga' ya ustaafu

Na Mwandishi MAALUM

**W**AZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, akiwa anatoa hotuba ya kuhitimisha bajeti ya ofisi yake ya mwaka 2024/25, alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Deogratius Ndejemi kuongeza wigo wa kusambaza elimu ya mafao kwa watumishi kwa lengo la kujenga uelewa wa kutosha.

Maneno haya ya Majaliwa ndio msingi mkubwa wa Tanzania kwa sasa, ambao wanahitaji elimu ili kuwa na utambuzi wa elimu ya kanuni za mafao kwa watumishi kupitia njia mbalimbali kama sehemu ya suluhisho na utulivu.

Elimu ni suluhisho, kama siyo leo, kesho. Naomba tuwe tunakumbuka kutoa elimu ya kustaafu, pindi mwajiriwa anapojiunga na mfuko wa hifadhi ya jami.

Kuwa na elimu ya mafao, kutawapa mwanya watumishi kujiandaa mapema. Wasijiandae jua likiwa tayari linakwenda kuzama. Ndio maana tunapata shida hivi sasa, kwani idadi kubwa ya wastaafu hawakupata elimu ya mafao wakiwa bado kazini ili wajipange vyema.

Iwapo wafanyakazi wangukuwa wametumia hekima yao kujiandaa kustaafu, wangetamani wapate pensheni nono ya kila mwezi inayoongezeka tu, ili iwasaidia kupata mshahara baada ya kufanya uwekezaji katika maisha yao ya ujana. Hii ndiyo maana halisi ya pensheni dhidi ya kiinua mgongo cha zamani.

Ni vyema pia, wabunge wote wasaidie wapiga kura kupanga maisha yao kwa hekima.

Kwanini China ni tajiri sana kwa sasa? Wanaikopesha hadi Marekani? China imepiga hatua kubwa ya kimaendeleo. Siyo kwa sababu ya wingi wao au kwa kuwa ni wafanyakazi hodari kama Wajapani, la hashai!

Wachina wamejenga utamaduni



*Deogratius Ndejemi*

wa kuweka akiba. Huu ni utamaduni unaostahili kuhamasishwa hapa Tanzania. Wanawekeza kwenye maeneo mbalimbali. Wanajiandaa kustaafu kwa heshima. Siyo eti wakistaafu, ndio waanze kubebana na mfuko ya simenti kwa ajili ya kujenga na kuanza maisha wakati maisha yanakaribia ukingoni.

Utafiti unaonyesha kuwa watu wenye pensheni nono huishi kwa amani na muda mrefu, kwa neema ya Mwenyezi Mungu, iwapo hawatapata ajali, kulinganisha na wale wanaochukua mafao ya mkupuo.

Kutokana na hali hiyo, ndiyo maana mataifa yaliyoanzisha mifumo hii ya pensheni ulimwenguni, yanaweka masharti magumu ya kuwazuia watu wao wasishawishike 'kukwapua amana' zao ili iwafae maishani, nguvu zikiwa zimepungua.

Huko kwao, watu wanastaafu, lakini wanapokea hadi silimia 86 ya mishahara yao. Hata ukikwapua au kumtapeli mafao ya mwezi mmoja, mwezi unaofuata hela inaingia kwenye akaunti. Maisha yanaendelea.

Hivi sasa kuna mjadala mkali kuhusu mafao ya wastaafu na hasa kikokotoo, kila mtu anakuwa na mtazamo wake, lakini lengo la serikali ni kuhakikisha wastaafu wanakuwa na maisha ya maana hata baada ya kustaafu kazini baada ya miaka mingi ya kulitumikia taifa.

# Chui mweupe...



Muonekano wa pekee wa jamii ya chui mweupe – wengine wakiwaita, simbamarara, ambao wanapatikana zaidi Bara la Asia, hasa maeneo ya mashariki mwa India na Bangladesh, siyo wanyama albino, bali jeni zao ziko hivyo. Inasemekana kwamba chui hao weupe hukua haraka na wazito kuliko wale wenye rangi za machungwa na nyeusi wanaopatikana zaidi Afrika. (Picha kutoka mtandao).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

